# Taswira ya Utandawazi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili: Mfano wa Riwaya ya *Dunia Yao*

Alex Umbima Kevogo

## Iksiri

Nyenzo kuu za kuenezea utandawazi ni lugha, fasihi yake, vyombo vya habari, muziki na tafsiri. Tunapozungumzia utandawazi tunazungumzia maisha yetu ya kila siku na lugha tunayoitumia katika elimu, mawasiliano na mazungumzo. Kwa upande mwingine, utandawazi ni mfumo wa kimataifa unaorahisisha mawasiliano na mahusiano katika nyanja za kiuchumi, kibiashara, na kisiasa uliojikita kwenye maendeleo ya teknolojia ya habari. Kwa hivyo lugha ya Kiswahili pamoja na fasihi yake ni nyenzo muhimu ya kuenezea utandawazi. Makala hii inahoji kuwa uchumi, biashara na siasa ni asasi muhimu ambazo huathiri maendeleo ya jamii. Taathira za asasi hizi hujitokeza katika lugha inayotumiwa kila siku katika elimu, mawasiliano, mazungumzo na fasihi. Matumizi haya ya lugha kimaandishi au kimazungumzo hudhihirika katika muktadha maalum wa utamaduni na mazingira ya jamii husika. Jamii imekubali mabadiliko ya sayansi na teknolojia na kuuruhusu uhusiano baina ya wanajamii uwe umeelekezwa kwenye fikra za maendeleo haya. Kwa hiyo, uhusiano wa fasihi na utamaduni wa jamii umekuzwa chini ya misingi ya maendeleo ya sayansi na teknolojia ambayo yamemtoa mwanajamii nje ya mipaka ya fikra finyu za utamaduni wake tu hadi ule wa kimataifa. Lugha inayotumiwa katika kazi fulani ya fasihi huathiriwa na kile kinachotokea katika jamii ya mwandishi. Mwandishi huchota fikra, maudhui, falsafa, itikadi, mtindo, maumbo na miundo lugha kutoka kwenye jamii hiyo hasa inapokuwa katika kasi ya mabadiliko. Lengo la makala hii ni kutathmini hali hii inavyojitokeza katika fasihi ya Kiswahili kwa kutumia mfano wa riwaya ya *Dunia Yao* ya S.A. Mohamed (2006).

## 1.0 Utangulizi

Riwaya mpya ya Kiswahili ilizuka mwanzoni mwa miaka ya 1990, sambamba na neno ‘utandawazi’ lilipoanza kutumika katika Kiswahili kuanzia miaka ya 1990 (Gromov, 2004; Khamis, 2004). Gromov (2004) anachunguza mabadiliko katika fasihi ya Kiswahili ambayo imechukua dhima mpya ya kushughulikia matatizo yanayoikabili dunia nzima ya sasa. Kwa upande wake, Khamis (2004) anachunguza mabadiliko yanayojitokeza katika riwaya tatu za Kiswahili zilizochapishwa miaka ya 1990 na kuendelea. Jumla ya riwaya za Kiswahili zinazoitwa mpya ni *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1990) za E. Kezilahabi, *Walenisi* (1995) ya K. Mkangi, na *Ziraili na Zirani* (1999) ya W. Mkufya. Nyingine ni *Babu Alipofufuka* (2001) na *Dunia Yao* (2006) za S. A. Mohamed, *Makuadi wa Soko Huria* (2002) ya S. Chachage, na *Bina-Adamu!* (2002), *Musaleo*! (2004), *Dharau ya Ini* (2007) na *Unaitwa Nani?* (2008) za K. W. Wamitila.

Miongoni mwa sifa za riwaya hii ni ile ya kushughulikia kwa kina matatizo yanayoikabili dunia ya sasa. Riwaya hii hushughulikia matatizo ya ndani ya nchi na jamii husika kwa kiwango fulani, lakini kwa kiasi kikubwa imekiuka mipaka ya kitaifa na kieneo na kuangalia hali ya mataifa ya ulimwengu kwa mfano tatizo la utandawazi. Riwaya hii inaakisi sifa za kisanii ambazo hazipatikani katika riwaya nyingine zinazobainika katika fasihi ya Kiswahili. Usanii huo unaweza kutokeza kwenye viwango tofautitofauti kama: Usimulizi, mitindo ya uashiriaji, matumizi

ya lugha, usawiri wa wahusika, matumizi ya mtazamo na kadhalika. Riwaya mpya pia inaonyesha sifa za kimtindo na kimuundo ambazo zinakiuka sifa zinazohusishwa na riwaya ya jadi.

Istilahi utandawazi ina utata mwingi kutegemea msisitizo wa anayeitumia. Wataalamu wengi wameitolea fasili mbalimbali na kuitumia kwenye miktadha tofauti (Simala, 2006; Mulokozi, 2006; Batibo, 2006; Masele, 2006; Kezilahabi, 2006). Hata hivyo, wanaafikiana kuwa ni neno linaloelezea mfungamano na uhusiano uliojitokeza miaka thelathini iliyopita; hasa katika biashara, uchumi na utamaduni miongoni mwa jamii tofauti za dunia. Utandawazi umepata kasi kubwa ya kuwekeza mitaji na kupata faida kubwa kiuchumi na kiutamaduni. Kwa upande mwingine, utandawazi unahusishwa na kuenea kwa tamaduni za Kimagharibi kwa njia ya kibiashara au kushamiri kwa picha kupitia video, televisheni, mitandao ya simu, sidii, dividii na visidi na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Mwandishi wa riwaya ya *Dunia Yao* ni Said Ahmed Mohamed Khamis aliyezaliwa Zanzibar mnamo mwaka 1947. Alisomea katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Karl Marx huko Leipzig, Ujerumani. Said Ahmed Mohamed ametunga kazi nyingi kama vile: *Dunia Mti Mkavu* (1980), *Utengano* (1980), *Sikate Tamaa* (1981), *Kina cha Maisha* (1984), *Kiza katika Nuru* (1988), *Pungwa* (1988), *Asali Chungu* (1989), *Tata za Asumini* (1990), *Kivuli Kinaishi* (1990), *Amezidi* (1995), *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000), *Babu Alipofufuka* (2001), *Sadiki Ukipenda na Hadithi Nyingine* (2002), na *Jicho la Ndani* (2002). Nyingine ni *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine* (2005), *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine* (2005), *Dunia Yao* (2006), *Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine* (2007), *Siku ya Siku na Hadithi Nyingine* (2008), *Nyuso za Mwanamke* (2010), *Mhanga Nafsi Yangu* (2012) na *Mkamandume* (2013). Riwaya ya *Dunia Yao* inaangazia taathira za utandawazi hasa katika mataifa ya Kiafrika. Riwaya hii inahoji manufaa ya utandawazi katika Bara la Afrika.

Taswira ni picha zinazotokana na maelezo ambayo yanapatikana katika matini fulani (Wamitila, 2008). Kuna taswira za kimaelezi zinazotokana na maelezo ya kwenye matini na taswira za kiishara ambazo zina ujumbe wa ziada. Taswira kuu katika riwaya ya *Dunia Yao* ni ile inayoonyesha picha ya taathira za utandawazi katika mataifa ya Kiafrika. Mwandishi amekuza taswira hii kupitia lugha yenye mnasaba wa utandawazi. Aidha, usimulizi wa riwaya unakiuka misingi ya kawaida iliyozoeleka jambo linaloangazia taathira za utandawazi katika masimulizi. Isitoshe, wahusika wanaosawiriwa kwenye riwaya ya *Dunia Yao* ni wale wanaokiuka misingi ya uhalisia jinsi inavyofafanuliwa kwenye makala. Dhana ya wakati katika riwaya imetumiwa kujenga taswira kuu ya utandawazi kwa sababu hatuwezi kuuweka katika ncha mbili za mwanzo na mwisho. Kwa upande mwingine, riwaya inajirejelea yenyewe na kumfichulia msomaji mbinu zilizotumiwa kuitunga. Hili linaangazia pia taswira ya utandawazi katika uandishi wa riwaya.

Makala hii imegawanywa katika sehemu kuu kumi. Sehemu ya kwanza ni utangulizi wa makala. Sehemu ya pili inashughulikia jinsi dhamira ya utandawazi inavyojitokeza katika riwaya ya *Dunia Yao*. Sehemu ya tatu inaangazia matumizi ya lugha kwenye riwaya. Sehemu ya nne inazingatia usawiri wa wahusika katika riwaya. Sehemu ya tano kwa upande wake inashughulikia suala la usimulizi. Kwenye sehemu ya sita, tumezingatia jinsi dhana ya wakati inavyojitokeza katika riwaya. Sehemu ya saba inazingatia hali ya ujirejelevu, nayo ya nane imejikita kwenye mwingilianomatini katika riwaya. Umbo la riwaya limejadiliwa kwenye sehemu ya tisa. Sehemu ya kumi ni hitimisho la makala.

## 2.0 Dhamira ya Utandawazi katika Riwaya ya *Dunia Yao*

Kuna mitazamo miwili kuhusu dhana ya utandawazi. Mtazamo wa kwanza huchukulia utandawazi kuwa na faida kubwa kwa nchi zote duniani, kwa sababu hatimaye utaboresha maisha ya watu wote. Mtazamo huu unadai kuwa utandawazi una manufaa kwa nchi zinazoendelea kwa sababu unafungua milango ya biashara, masoko huria ya bidhaa na kuufanya utamaduni wa taifa moja ukutane uso kwa uso na utamaduni wa mataifa mengine (Ruigrok na Van Tulder, 1995).

Mtazamo wa pili unakanusha madai haya kwa rai kuwa utandawazi ni upeo wa dhana kongwe yenye sifa mpya ya kutumia maendeleo makubwa yaliyopatikana kiteknolojia, kunyonya utajiri na rasilimali za dunia na kuwaacha watu wa mataifa maskini kuwa fukara zaidi, kunajisi uchumi, tamaduni, mazingira na maisha yao vibaya kiasi kwamba nchi hizo hudharauliwa na kuonekana kuwa duni katika fikra ya dunia ya sasa. Mtazamo wa pili ndio unaotawala katika riwaya ya *Dunia Yao*. Katika riwaya hii, taathira za utandawazi zimesawiriwa kutokana na matatizo ya kiuchumi ya mataifa yaliyotokea miaka ya 1970, ambayo yalisababishwa na maslahi ya kibiashara na utashi wa mataifa yaliyopata ufanisi mkubwa yanayolenga kila siku kupata faida kubwa.

Mwandishi wa riwaya hii anapinga madai kuwa utandawazi una faida yoyote kwa mataifa ya Dunia ya Tatu. Mwandishi anaelekeza hasira zake kwa kile ambacho anakiona kuwa ujinga wa viongozi wa nchi za Dunia ya Tatu kukubali kiholela kuziuza nchi zao kwa mataifa makubwa. Mwandishi anatuchorea taswira kuu ya taathira za utandawazi kupitia kwenye picha ndogo zenye kuibua hisia za chuki, kero na chukizo. Utandawazi umedhihirishwa kuwa ni nguvu zinazodhibiti, zinazodhulumu na zenye kuangamiza; nguvu hizi ndizo zinazomsukuma binadamu kufanya kila ovu. Mwandishi anasawiri nguvu za sayansi na teknolojia ambazo zimekuza utashi wa pesa, vitu, bidhaa na ubinafsi. Mwandishi analinganisha nguvu hizi na dini mpya inayoitawala dunia ya sasa. Dondoo lifuatalo linathibitisha hali hii:

> ...Hivi viji-Ungu vidogo ndivyo vinavyounda dini mpya. Ndivyo vinavyotawala hivi leo-sayansi, teknolojia na utashi wa pesa ndiyo msingi wa dini yetu mpya. Ndizo nguvu zinazotamba hivi leo (Mohamed, 2006: 48).

Dondoo hili linasawiri nguvu za utandawazi ambazo ziko nje ya uwezo wa kila mtu. Utandawazi umeonyeshwa kama nguvu zinazotawala ulimwengu wa sasa. Nguvu hizi zimegubikwa ndani ya sayansi na teknolojia na uwezo wa kiuchumi unaoendesha kila kitu duniani sasa. Utandawazi unasawiriwa kuwa na nguvu za kiungu zinazotawala na kuiendesha dunia ya sasa.

Taswira ya utandawazi kama nguvu zinazodhibiti, zinazotawala na zinazoongoza dunia ya sasa inajitokeza kupitia mataifa saba yenye uwezo wa kiuchumi na ushawishi wa kisiasa 'yaliyo na uwezo wa kuvamia, kunyonya rasilimali na kuyaibia mataifa ya Dunia ya Tatu.' Mataifa haya saba, yakishirikiana na vyombo kama Benki ya Dunia, Shirika la Fedha Duniani na Shirika la Biashara Duniani yanatumiwa kutoa mikopo kwa masharti magumu ili kuendeleza dhuluma na ukandamizaji wa mataifa maskini. Hali hii inabainika wazi kupitia kwa dondoo lifuatalo:

> ...Unapigana kuondoa umaskini duniani. *New World Order, WTO, Globalization*-kipanya na ndovu wanaposhindana nguvu. Unapigania haki za binadamu. Iraki na Kuwait. '*Sanctions*' kiboko kwa wasiofuata...Fedha. Fedha. Fedha. Pesa. Pesa. Pesa. Misaada. Misaada. Misaada. Mikopo. Mikopo. Mikopo. Haihatarishi uhuru wetu! (Mohamed, 2006:46).

Dondoo hili linaonyesha jinsi mataifa ya Kiafrika yanavyobebeshwa mzigo wa masharti magumu baada ya kupokea misaada na mikopo kutoka kwa mataifa ya kigeni. Mataifa ya Kiafrika hayana uwezo wala nguvu. Mataifa haya yanalinganishwa na panya anayeshindana nguvu na ndovu. Hii ina maana kuwa yamepoteza uhuru na yanaendelea kutawaliwa kutoka mbali kupitia kwa nguvu za utandawazi.

S.A. Mohamed (2006) anaonekana kusikitishwa na hali ya dunia kuwa moja, yaani kijiji kimoja. Kijiji hiki chenye wepesi wa mawasiliano kimekolea utamaduni wa kigeni anaoulinganisha na sumu. Taswira hii inayoonyesha dunia ya sasa (*Dunia Yao*) kama uwanja wa fujo inabainika wazi kwenye dondoo lifuatalo:

> Fujo. Fujo tu! Ukweli ni kwamba dunia imekuwa moja vibaya mno kwa sababu ya usahili wa uwazi wake na wepesi wa mawasiliano na utashi wa kudhibiti. Taathira ya utandawazi. Mbaya kiasi kwamba hakuna tena mipaka ya maafa, lakini kuna mipaka ya raha. Yakitokea maafa pahala pamoja huenea duniani kote. Mazingira yamepotoka. Utamaduni tusiotaka hatuwezi kuuzuia tena. Unakuja kwa mawimbi yenye nguvu. Ngono, ulevi, uchi, matusi, kelele, mavazi ya kuchekesha...Na miili yetu inajazwa sumu (Mohamed, 2006:48-49).

Kwa mujibu wa dondoo hili, dunia hii mpya isiyojali mipaka inasheheni kila aina ya uozo. Kuna vyakula vilivyotengenezwa kwa utaalamu wa sayansi na teknolojia ya kisasa vilivyojazwa sumu. Kuna ongezeko la madawa ya kulevya, wimbi la wakimbizi linalotishia amani duniani, taathira ya vyombo vya habari na mawasiliano vinavyosambaza uhalifu, uwongo na unafiki. Kuna dini zinazoshadidi upya na wafuasi wanaoburururwa bila kufikiri. Vikundi vya maharamia na wahalifu vimepata nguvu. Isitoshe, ukatili unavunja hisia za vijana na kuwafanya wauaji.

Ukatili huu unatokana na michezo ya kikatili ambayo vijana wanaiona kwenye sinema na silaha zilizotapakaa kila mahali na kuuzwa kiholela.

Nguvu za maangamizi ya utandawazi zinalinganishwa na wimbi kubwa la fikra mpya zinazombadilisha binadamu kwa kasi isiyoeleweka. Nguvu hizi zimemwelemea na kumkandamiza binadamu. Utandawazi unalinganishwa pia na pepo zivumazo kwa kasi na kutifua vumbi linalokivaa kila kitu na kukigeuza. Utandawazi unalinganishwa na kimbunga kinachomsukuma, kinachomrusha na kumwangusha chini binadamu bila hiari yake. Taswira kamili inajitokeza kwenye dondoo lifuatalo:

> El Ninyo amezaliwa. Naye siku hizi kuliko zamani, hudandisha jua ili ardhi ichanike vipandepande. El Ninyo hanyeshi tena mvua tu! Sasa na jua pia! Hakuna kinachomea ndani ya tanuri lake. Ukitembea utababua miguu yako ya bata bure! Akichoka kuangaza jua, El Ninyo huangusha vua za kuangamiza kila kitu katika mafuriko...Akichoka kunyesha hachelei tena kupiga zilzala na kukariri, mara hapa mara kule (Mohamed, 2006:65).

Kwenye dondoo hili dunia ya sasa inayoshuhudia mabadiliko ya kila aina; inamithilishwa na tanuri. Kila kitu kinasawiriwa kuwa kinawaka moto. Mabadiliko ya tabia-nchi na hali ya anga yanayosababishwa na uharibifu wa mazingira yanaonekana bayana. Hali hii imesawiriwa kupitia istilahi ‘El Ninyo’ ambayo ni taashira ya uharibifu wa mazingira unaoenda pamoja na utandawazi. Nguvu za uharibifu za utandawazi zinalinganishwa na tukio la El Ninyo ambalo husababisha mafuriko.

Utandawazi umesheheni ugeugeu au unyume wa aina fulani. Wazo kuu linalotawala hapa ni kuwa, ‘ukidhaniacho ndicho kumbe sicho.’ Mwandishi anatuchorea picha ya bustani ya ajabu ili kuuelezea ugeugeu wa utandawazi. Kila kitu ndani ya bustani hii ni cha kisuriamasuriama. Taswira hii inalenga kuonyesha uzuri wa mkakasi ndani pande la mti unaoendana na utandawazi. Kila kitu barani Afrika kinasimamia nguvu za nje ambazo zimejificha ndani ya gamba la Uafrika. Wanaoendesha biashara barani Afrika ni wawekezaji kutoka kwenye mataifa makubwa. Wageni wanaendesha shughuli zao chini ya mikakati ya Mataifa Saba yenye uwezo mkubwa kiuchumi duniani, Benki ya Dunia, Shirika la Fedha Duniani na Shirika la Biashara Duniani; vyombo vinavyosimamia, kuimarishwa na kuendelezwa na itikadi ya uliberali-mpya. Kuhusu ugeugeu wa utandawazi, mwandishi anajenga picha ifuatayo:

> ... hii ilikuwa bustani ya ajabu. Kila kitu ndani yake cha kisuriamasuriama. Cha kiTshombeTsombe. Cha kimulatomulato. Kila kitu kimepandikizwa na kuundwa *ki-hybridhybrid*...Mafuta mazuri yanatoka Uzunguni. Moshi wa vipando unaoingia na kukorokocha mianzi ya pua. Kutuzi la watu wanaozidi kusongamana. *Skyscapers* zinatoka nje kuja kuotesha hapa. Zinaotesha bega kwa bega na vibanda vya mgongo (Mohamed, 2006:66).

Hali ya kuchanganya mambo na pia tamaduni kutoka katika maeneo yote ya dunia inabainika kwenye dondoo hili. Picha hii inayoonyesha bustani iliyo na vitu vya rangi mbalimbali; ni picha ya dunia ya sasa. Dunia hii ni jungu kuu la kuyeyushia tamaduni zinazoibuka kote ulimwenguni. Matokeo yake ni dunia isiyoeleweka na iliyokosa utambulisho. Taswira za uoni na zile za hisi kupitia kunusa zimetumiwa kuchora picha hii. Kuna kutuzi (harufu mbaya) na moshi unaokera puani katika mandhari haya. Lengo la kutumia taswira hii ni kuibua hisia za kukera kuhusu suala zima la utandawazi.

Mohamed (2006) anaposawiri taathira za utandawazi anatumia lugha ya uhakiki na mkemeo kwa utandawazi. Lugha hii inakita katika kauli, picha na jazanda zinazojenga kejeli na tashtiti; kisha anaikuza taswira kuu inayodhihirisha taathira za utandawazi. Matumizi ya tashtiti yanalenga kufichua na kushambulia ujinga, ujuhali na upumbavu wa jamii na uongozi wao na uchungu walionao kwa ujinga huo unaotendeka. Hali hii inadhihirika wazi kwenye dondoo lifuatalo:

> ...wamechukua kila kitu...wao wamekuwa ndio wafikiri wetu, wasemaji wetu, wanaohisi kwa ajili yetu, wanaona njaa na kiu zetu...kwa ujumla wanaendesha maisha yetu....kwa ufupi wao ni kila kitu. Sisi wengine ni mapipa matupu. Hatuna rojo la uhai: Hatuna supu ya maisha wala nyama ya ubinadamu wetu. Hatuna sehemu ya utu.... Hatuna chetu. Hatuwezi kufikiri kama wao au zaidi ya wao. Hatutarajiwi kusema. Hatutarajiwi kushiriki hata mambo yanayohusu nafsi zetu.

Katika dondoo hili mataifa ya Kiafrika yanakejeliwa kwa kuyaruhusu mataifa ya kigeni kufikiri kwa niaba yao. Wenyeji wa mataifa ya Kiafrika wanalinganishwa na mapipa matupu; picha inayobainika hapa ni ile ya kuweza kusukumwa popote kwa urahisi. Tashtiti imetumiwa kukemea ujinga wa mataifa ya Kiafrika wa kuyaruhusu mataifa ya kigeni kuumiliki utu wao na kuwanyima uhuru wa kushiriki katika mambo yanayowahusu.

Utandawazi umesawiriwa kusheheni utata na mkinzano wa mambo. Isitoshe unasheheni nguvu zinazovunjavunja na kuharibu kila kitu. Binadamu ameumbuliwa kiasi kwamba amekosa utambulisho wake jinsi muundo wa riwaya ulivyoparaganyika. Utambulisho wa watu umevunjika na kuharibika katika viwango vya kibinafsi, kitaifa, kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kidini. Mtu binafsi amevunjikavunjika kwa sababu hana pahala pa kusimama katika kudai haki zake za kimsingi kama vile kupata kazi ya kumwendeshea maisha yake kwa sababu utandawazi umevuka mipaka na kuchukua vyombo vya taifa na kuvitia katika mitaji na utajiri au maslahi yao. Viwanda, benki na rasilmali za nchi zimenyakuliwa na kuhodhiwa. Mwandishi ameisawiri hali ya kuvunjikavunjika kwa utambulisho wa mtu binafsi kupitia kwa mhusika mkuu Ndi- anapoilalamikia hali yake:

> ... Labda nipo. Pengine sipo! Tofauti gani? Ndiyo, moyo bado unatuta. Hii labda ndiyo ishara ya pekee iliyobaki. Pangaboi linapepea pasi na nguvu za umeme. Kishumaa kidunya kinadidimia na kujitahidi kunilaza salama. Sijui lakini lini?

> Mwaka gani? Mwezi gani? Siku gani? Saa? Wakati hauwaziki tena. Mashiko hauna mantiki umeachana. Umepoteza maana! Saa inatiktika mezani. Inasonga mbele. Aaaa saa! Chombo tu na namba zake (Mohamed, 2006:1).

Utambulisho wa kibinafsi wa mhusika Ndi- umevujikavunjika katika dondoo hili. Ndi- hajui iwapo yupo au hayupo kumaanisha kwamba amekosa utambulisho katika dunia ya utandawazi. Kinaya cha haya yote ni kwamba haoni tatizo lolote katika hali yake ya kukosa kujitambua. Ndi- analinganishwa na pangaboi na anaendeshwa na upepo wa utandawazi. Isitoshe, amekosa kutambua wakati; hajui anaishi lini. Hii ina maana kwamba nguvu za utandawazi zinazomwendesha kwa kasi zimeufanya wakati kukosa mantiki na umuhimu kwake.

Utandawazi umevunjavuja utambulisho wa mataifa kwa kuyapokonya nguvu na uwezo wa maamuzi ya nchi kiuchumi na kijamii. Utambulisho wa kitaifa hauna umuhimu tena, utandawazi umeugawa ulimwengu katika matabaka; yaani Dunia ya kwanza, Dunia ya pili na Dunia ya tatu. Nchi lazima zifuate masharti ya vyombo vinavyotetea utandawazi kama vile Shirika la Fedha Duniani, Benki ya Dunia na Shirika la Biashara Duniani. Nchi za Dunia ya Tatu hazina tena sauti sio tu katika mambo ya kiuchumi bali pia katika yale ya kisiasa na ya kidunia. Taswira hii inajitokeza katika dondoo lifuatalo:

> ... kila kitu katika maisha kimevunjika vipandevipande na maisha yenyewe yanakwenda mbio ajabu. Kasi, kasi, kasi ya umeme iliyoanzishwa kwenye kiwanda cha *Ford*, *Microsoft* na *McIntosh*. Ukifumbua macho utaona picha ya wenye mfumo huu wakiwa katika chombo fulani cha ajabu wakisukuma na kuwalazimisha watu wengine kudandia chombo chao-chombo cha waungwana. Tazama mgawiko huu: dunia ya kwanza, ya pili na ya tatu (Mohamed, 2006:171).

Katika dondoo hili majina ya viwanda vya kigeni yametumiwa kwa makusudi na mwandishi ili kuonyesha ukoloni mamboleo unaoendelea Afrika. *Ford*, *Microsoft* na *McIntosh* ni viwanda vya Marekani vinavyoendesha biashara duniani na hasa barani Afrika kwa kiwango kikubwa. Uwezo wa viwanda hivi kudhibiti biashara duniani kupitia kwa mifumo ya kiukiritimba inabainika wazi. Kiwanda cha *Microsoft* kitengenezacho programu za kompyuta ni kielelezo cha ukiritimba duniani. Kila mtu hulazimika kununua programu zao kwa sababu ndizo zilizopo kwingi duniani. Udhibiti wa aina hii unalipa taifa la Marekani na viwanda vyake ushawishi mkubwa kiuchumi duniani.

Utandawazi umesawiriwa kwa picha za kimiujiza na zenye kustaajabisha. Utandawazi unaoneshwa kama pandikizi la jitukitu lililo na umbo lenye utata na lisiloeleweka. Utandawazi una nyuso nyingi zinazobadilikabadilika. Uzuri wake unapendeza lakini unasheheni hatari ya maangamizi. Dondoo lifuatalo linaakisi hali hii:

> ... Kitu au jitu? Utata wa kijitukitu labda. Umbo lake limekasmika nusu kwa nusu, kushoto na kulia, katikati ya jimwili lake. Pandikizi la jitukitu jinsi lilivyoumbika. Kushoto linamemetuka anga la ki-Ungu linaloumiza macho na kuogofya. Kushoto pia lilikuwa limechanua uzuri wa ajabu. Uzuri wa kike ndani

> ya uzuri wa kiume. Uzuri unaokanganya. Sijapata kuona kiumbe duniani chenye uzuri namna hii. Useme hao huru-l-'ayn wa peponi watajikanao. Na kulia jimwili lake limekumbatiwa na giza zito la maangamizo ambalo kila mara lilikuwa likiripuka moto kuunguza kila kitu kilichosimama kwenye njia yake. Lilikuwa likipita kwa kasi ya umeme, lakini bado lilionekana lipo papo hapo daima-haliondoki! linapiga kasi katika njia yake inayojiandika yenyewe-mara *Globalization* mara *Americanization*. Na lilipotimka lilitifua kila kitu kilipojaribu kufukuzana nalo, kilijikuta kinaachwa nyuma milioni ya kilomita. Likipita kwa kasi na pepo zake za dhoruba likilipuka madimi ya moto yaliyounguza na kukausha kila kitu...(Mohamed, 2006:205-206).

Hali ya utandawazi kuwa na utata inabainika wazi kupitia kwa taswira ya jitukitu inayojitokeza katika dondoo hili. Uhakika iwapo ni jitu au kitu haujulikani bayana. Kuna ukinzani kuhusu umbo, mwonekano na vitendo vya jitukitu hili. Hali hii inabainika kuwili, lina upande wa kushoto unaopendeza na wa kulia unaotisha na kuogofya. Jitukitu hili linapita kwa kasi japo lipo hapohapo daima. Haijulikani iwapo jitukitu hili ni utandawazi au Umarekani duniani; ni vigumu kutenganisha haya mawili. Lengo la mwandishi hapa ni kuonyesha ugiligili na ugeugeu wa utandawazi unaoufanya kuwa mgumu kuelezeka.

Utandawazi umesawiriwa kama nguvu zinazovunjilia mbali mipaka ya mataifa na kuigawa upya dunia katika sehemu mbili kwa misingi ya utabaka unaotegemea uwezo wa kiutawala na nguvu za kiuchumi. Kwa upande mwingine, utandawazi unajitokeza kuwa chanzo cha kudhoofika kwa maadili katika jamii za ulimwengu hususan Afrika kwa kusababisha ufisadi, wizi na ukahaba. Kuhusu hali hizi mwandishi anatujengea picha ifuatayo:

> ... dunia hii ya leo ina maharamia wa aina nyingine, kama vile kwa mfano, wanaonunua dhahabu kwa kulipa asilimia 5 ya mapato yote ya machimbo na kuchukua asilimia 95. Kuna wanaouza dhahabu na kununua maradhi ya watu wao...(Mohamed, 2006: 96).

Dondoo hili linaonyesha kukosa maadili na dhuluma zinazoongoza biashara ya kimataifa. Makampuni ya mataifa ya kigeni yaliyoingia mikataba na mataifa ya Kiafrika ili yachimbe madini hutumia dhuluma kunyonya rasilimali hizi. Asilimia kubwa ya mapato yatokanayo na uchimbaji huu hupelekwa katika mataifa ya kigeni huku yale ya Kiafrika yakipokea malipo duni. Maeneo yanayochimbwa madini haya ni hatarishi na chanzo kikubwa cha maradhi yanayowasibu wakaazi wa sehemu hizo.

Mwandishi wa riwaya ya *Dunia Yao* ameshughulikia taathira za utandawazi ambazo zimesababisha matatizo ya kisaikolojia, kijamii, kiuchumi na kisiasa duniani na hasa barani Afrika. Mkondo mzima wa hali ya binadamu kubadilika umechunguzwa kupitia kwa mchanganyiko wa visaasili, migani, na hurafa chini ya utaratibu wa mwingilianomatini.

## 3.0 Lugha katika Riwaya ya *Dunia Yao*

Lugha ya riwaya mpya ya Kiswahili ina *mvutogubi*[1] na ugumu wa aina fulani unaotokana na matumizi ya mafumbo, visasili, migani na matukio ambayo hayakamatani na mantiki tuliyoizoea. Kwa mfano, ili kutuonyesha shengesha ya utandawazi ambao umesababisha umaskini na unyonywaji wa mataifa maskini unaoendelezwa na mataifa makubwa, mwandishi anatoa taswira ifuatayo inayoibua hisia za chuki:

> Tangu kuzaliwa sijapata kuona mahali pachafu kama hapa. Vibanda vimechipuka ovyo. Labda vibanda si neno zuri, kwani huku kwetu, kibanda kilikuwa na sura na heshima yake. Hivi ni vichafukizi vilivyosimamishwa na shaghalabaghala mpya. Vilivyojengwa kwa kitu chochote. Chochote kisichofaa-kinachofaa: *ma*gogo, fito, papi, *ma*tambara, mibacha, *ma*jamvi *ma*bovu, *ma*boksi, *ma*pande ya *ma*bati yenye kutu, *ma*salia ya *ma*debe yaliyochoka, mbao zilizokwisha mung'unyuliwa na mchwa, *ma*jani ya miti...vyote vichafukizi vimesimama katikati ya tonge la taharuki za kila aina: *m*pacha*no*, *m*kurubia*no*, *m*kimbia*no*, *m*fukuza*no*, *m*didimiza*no*, *m*kengeuko, *m*titimo... (Mohamed, 2006: 32) (msisitizo kwa kuweka italiki ni wetu).

Maelezo ya mwandishi katika dondoo hili yanabainisha matumizi ya lugha yasiyo ya kawaida katika usimulizi wake. Lugha hii ni ya kishairi iliyo na takriri ya maneno na silabi za baadhi ya maneno. Kwa mfano, ili kuonyesha uduni wa mitaa ya mabanda inayochipuka kila mahali inayojengwa kwa vitu duni, mwandishi ametumia uradidi wa kiambishi **ma-** cha idadi ya wingi kwenye vifaa vinavyotumiwa katika ujenzi huo. Isitoshe, kuna takriri ya silabi ya kwanza kwenye maneno yanayotumiwa kusisitiza hali ya kujenga vibanda hivyo vibovu. Silabi zinazorudiwarudiwa katika maneno haya ni ile ya kwanza, yaani **ma-** na ya tamati **-no**.

Lugha inayotumiwa katika riwaya ya *Dunia Yao* ni ile inayojipambanua kwa *utouzowefu*[2] wake. Ni lugha inayokusudia kumvuta msomaji kwa jinsi inavyojitokeza kwanza kabla haijaibua maana. Mfano wa matumizi ya lugha ya aina hii unabainika katika dondoo lifuatalo:

> ... sasa dunia ilikuwa tanda, wazi, inang'ara kama bintiurejua. Mbele yangu lilitandizika sinia kubwa la ardhi... (Mohamed, 2006:179).

Neno 'utandawazi' katika dondoo hili limegawanywa katika sehemu mbili yaani 'tanda' na 'wazi'. Matumizi haya japo ni ya kawaida lakini yanatoa maana tofauti. Maneno haya yametumiwa kama vivumishi ili kufafanua zaidi nomino 'dunia'. Kwa kufanya hivi, tunapata taswira ya dunia ambayo imekuwa kijiji kimoja;

---

[1] Tafsiri ya neno '*Hermetic*' linalomaanisha mjazo wa jazanda zenye fumbo, nguvu na mapigo ya kimuziki ambayo mara kadhaa huonekana ni muhimu zaidi kuliko maana ingawa katika riwaya hii maana bado inabaki kuimarishwa (Khamis, 2004).

[2] Tafsiri ya '*Defamiliarisation*' ambayo ni tafsiri ya '*Ostranenie*' neno la Kirusi lililoanzishwa na Viktor Shklovsky. Hili ni neno lililoanzishwa na Shule ya Urasimukanuni lenye kubeba maana na kazi maalumu katika fasihi. Kazi ya kuichangamsha na kutia lugha uvuguvugu ili ionekane mpya au ngeni kuliko ilivyokuwa, lengo kubwa likiwa kubadilisha mtazamo wa msomaji kwa kumuonyesha ujumi wa lugha ambao utachukua makini ya msomaji, kumvuta kisanaa na kumfanya afikiri zaidi. Ni mchezo wa lugha (Khamis, 2004).

imeenea bila mgao wa mipaka. Hali hii inaonyesha kuwa hakuna tena vizuizi vya kitaifa wala kimasafa vinavyomdhibiti mtu kutangamana na mwenzake aliye mbali.

Mwandishi anatumia lugha inayokwenda vyema na *uhalisiamazingaombwe*[3] unaojengwa katika riwaya hii na ambao unakwenda vyema na maudhui yake na kile kinachotokea nje ya matini kwenye jamii hasa kuhusu utandawazi. Katika riwaya ya *Dunia Yao*, mazingaombwe yamesawiriwa katika ile hali ya mhusika mkuu, Ndi- kuikimbia nafsi yake, familia yake, marafiki, majirani na jamii kwa jumla; ile hali ya kuporomoka kwake na kuwa mwendawazimu anayeishi kwenye chumba kidogo mfano wa jela ambamo anazurura katika dunia pana bila kuzurura. Mwandishi anaieleza hali hii jinsi inavyobainika kwenye dondoo lifuatalo:

> ... sikuwa na mwingine wa kusema naye katika hii dunia ndogo, ndani ya kijumba hiki kama jela, humu nilimojikomelea mimi mwenyewe kwa hiyari yangu (Mohamed, 2006: 2).

Kwenye chumba hiki kinachoakisiwa katika dondoo, Ndi- anazurura katika ulimwengu wa ndoto. Katika dunia hii, anapanga udugu na kompyuta, mtu-mashine pekee aliyebaki katika maisha yake anayeweza kumwamini, kuzungumza naye, kushauriana naye, kutumia kama kiwango cha kuandikia historia na hadithi yake na hadithi za watu wengine na kiwambo cha kuweza kuzungumza na binti yake ambaye anaishi *London* kama mkimbizi. Mwandishi anaisawiri hali hii kupitia kuhuishwa kwa kompyuta kama inavyodhihirika katika dondoo lifuatalo:

> ... sasa nitakuwa na mwenzangu zaidi wa kusema naye. Huyu kompyuta nakusudia. Na si kusema naye tu, bali kufungamana naye kivitendo. Kiumbe cha kutegemea kunifungulia milango ya kusema na wengine (Mohamed, 2006: 8).

Sauti inayosikika katika dondoo hili ni sauti ya nafsi ya Ndi-. Hapa Ndi- anairai nafsi yake kwamba amempata mwenzake wa kusema naye, yaani kompyuta. Taswira inayojengeka hapa ni ya mtu mpweke aliyejitenga na kuchagua kuishi katika ulimwengu wake wa ndoto. Kompyuta ni taashira ya utandawazi na humwezesha mtu kutangamana na watu wengine wanaoishi mbali sana. Hali hii hurahisishwa kupitia mitandao ya kijamii ya intaneti na hata barua-pepe.

Katika riwaya kuna matambiko yanayohusishwa na Miungu ya Kiafrika kama ile ya kosmolojia ya Waibo wa Nigeria. Kwenye tambiko hili kuna mizuka wanaowakilisha ukale na miungu wa jamii hii wanaozungumza na kutenda kama binadamu wa kawaida. Mwandishi anaisawiri hali hii katika dondoo lifuatalo:

> ... mimi ni wengi katika mmoja, mjumbe wa Bwanamkubwa. Ni Orumali; msaidizi wa shani yake Bwanamkubwa. Nafahamu lugha zilizomo kichwani na hisia zenu za uwongo zilizomo nyoyoni. Ni Orisa-nla, mtunzi wa utenzi wenu...Ni Esu, mkaguzi wa mwenendo wenu katika haki na dhuluma...ni Sango,

[3] Tafsiri ya neno la Kiingereza '*Magical Realism*'. Pia, uhalisiajabu. Ni aina fulani ya fantasia, lakini ni mbinu inayozileta dunia mbili pamoja za 'ukale' na 'usasa'-ukale wenye misingi ya mazingaombwe au ukweli ambao hauwezi kuelezeka katika mantiki ya nchi za Ulaya. Na usasa unaojaa taathira za kiutamaduni, kisayansi na kiteknolojia iliyoletwa na wakati wa ukoloni na wakati baada ya ukoloni (Khamis, 2004).

> huamrisha ishara ya maangamizo ya radi...Ni Sopono, ninayeleta magonjwa...Ni Ogun ninayekata na kupita kwenye utupu wa mpito na kurejea tena duniani... (Mohamed, 2006: 192).

Majina yanayotumiwa katika dondoo hili yana mnasaba na jamii za Kiafrika zinazopatikana nchini Nigeria. Miungu wanaotajwa kama vile Ogun, Orumali, Sopono, Orisa-nlu na Esu ni wa jamii za Nigeria. Lugha ya aina hii inalenga kuonyesha wazi utamaduni na hali halisi ya maisha katika jamii za Kiafrika anazozisimulia mwandishi. Utamaduni unaosawiriwa unaakisi sanaa ya Mwafrika, shughuli zake za kijamii na imani yake ya kidini.

Mohamed (2006) anatumia *Kanivali* kuitashtiti hali ya bara la Afrika kukubali athari za kigeni na pia kushawishika kwa urahisi kuupokea utamaduni wa kigeni. Wafula na Njogu (2007) wanaeleza kuwa kanivali ni sherehe ya kitamaduni ambapo watu hujivisha katika mafigu yanayoficha sura zao. Wakiwa katika hali hii watu huigiza nyadhifa zisizokuwa zao. Miongoni mwa sifa za kanivali ni kuigiza kwa ububu, ubaradhuli na upumbavu katika mazungumzo. Mohamed (2006) amelisawiri bara la Afrika likiigiza tamthilia isiyoifahamu kwenye sherehe ya kanivali ya utandawazi. Bara la Afrika limekosa utambulisho kwa kuiga tamaduni, dini na itikadi za siasa za kigeni. Picha hii inajitokeza katika dondoo lifuatalo:

> ...hili la leo lakini lilikuwa sherehe la ndovu kumla mwanawe. '*Carnival*' la sherehe yake!...Tena likafuata kundi la wananchi wa kawaida. Hawa wote walionekana watu wa ajabuajabu. Ama warefu kama mnara wa *wireless* au wafupi kama ngiri...wote wamevaa kichekeshokichekesho na kimzahamzaha-kifensi yaani. Wengine wamevaa kama Mao, wengine kama Lenin, wengine kama Gandhi. Kuna waliovaa ki-Churchill au kirais wa US. Wengine *ki-Cowboy* au *ki-Western*...Wote wanapita wakicheza na kuimba wimbo wa Washington DC. Baadhi wamevaa ki-Rome ama wakiimba kasida za Vatican au wanabeba magunia ya unga na makoronya. Wengine wamevaa hagali za Kiarabu wanapita wakibwata Allahu Akbar! (Mohamed, 2006: 175).

Kanivali inayosawiriwa katika dondoo hili inalenga kukashifu uigaji wa mambo ya kigeni unaoendelea barani Afrika. Mwandishi anazingatia chanzo cha kasumba ya kuthamini na kung'ang'ania kitu chochote kile chenye asili ya kigeni. Kupitia tashtiti anakashifu uigaji wa itikadi za kisiasa zinazopwaya na zisizofaa katika muktadha wa Kiafrika. Imani za kidini zenye asili ya kigeni zinasawiriwa kama vyanzo vya kumkengeusha Mwafrika. Kwa ujumla lugha ya riwaya mpya ya Kiswahili inaakisi mnasaba na utandawazi. Lugha hii imekusudiwa kuukemea utandawazi na kuonyesha wazi taathira zake. Dhima hii inatekelezwa kupitia hisia za ghadhabu, hasira na kukata tamaa zilizobainika katika msamiati unaoteuliwa kwa uangalifu na mwandishi.

## 4.0 Wahusika

Wahusika wanaobainika katika riwaya ya *Dunia Yao* ni wale waliojengeka kwenye misingi ya usasabaadaye. Wahusika hawa ni vivuli vya watu au ni dhana zinazopewa uhai ili kusimamia kwa matendo dhamira, hoja, mtazamo na falsafa ya

mwandishi. Ingawa ni wahusika wenye sifa za kibinadamu, si wahusika ambao wanasadikika kimantiki.

Baadhi ya wahusika ni vizuu au maiti wanaofufuka, wengine ni mitume wanaorudi tena duniani. Wengine ni watu wa miujiza tu wanaoishi karne kwa karne bila ya kufa wala kuzeeka. Ni watu wenye uwezo wa kuisukuma milima. Wenye uwezo wa kupenya na kuishi ardhini au majini. Kuna wengine wanaochorwa kwa sifa za kiungu. Wengine ni wahusika wa jinsi mbalimbali wanaowekwa pamoja kwa haja ya mwandishi kuelezea dhana fulani ya kusisitiza ile dhamira ya umataifa. Kwa mfano, kuna hali ya kuonekana na kutoweka kwa mhusika wa kiajabu Muse au Mize, ambaye ameazimwa kutoka fasihi ya Ugiriki ya kale. Jina Muse, *limeswahilishwa* na mwandishi kuwa Mize ili kuwiana na muundo wa Kiswahili ilikojikita hadithi ya *Dunia Yao.*

Mhusika Mize anasawiriwa kwenye riwaya mwanzoni akiwa kama dhana kwenye akili na kumbukizi za Ndi-. Hata hivyo, wakati huohuo anao uwezo wa kujipa mwili na kuonekana na Ndi- kama mwanamke wa kutamanisha. Aidha, licha ya kwamba ana mbawa kama malaika au ndege, Mize ni shabaha ya uchu wa Ndi-. Ndi- anatamani sana kufanya ngono naye. Mize ndiye anamwelekeza Ndi- kwa kukaidi mpito wa nyakati na mipaka ya pahala, mipaka kati ya roho na mwili, mpaka kati ya kuwapo na kutokuwapo, mpaka kati ya kuonekana na kutoonekana, mpaka kati ya ukoloni na baada ya ukoloni, na mpaka kati ya Ugiriki ya kale na Uswahili.

Mwandishi ametumia visa vingi vya kimazingaombwe ambavyo vina wahusika picha katika riwaya yake. Mathalani, katika kipindi fulani Ndi- anapokuwa anapitia albamu ya aila yake, picha za washiriki wa aila zinahuishwa na kutoka kwenye albamu, na kisha hao washiriki wa aila wanatenda na kutendana kihalisi kama kwamba albamu imegeuzwa kiwambo cha sinema ambapo kila mhusika anatekeleza jukumu lake kwenye maigizo. Kwa hiyo, msomaji anajikuta anashuhudia igizo ambalo linamshirikisha Ndi- kama mtazamaji na pia mhusika. Wakati huohuo, washiriki hao wa familia wanatangamana na Ndi- anayeitazama albamu, wakisemezana, kutenda na kutendana wao kwa wao au kutendana na msimulizi. Mfano wa kuibuka kwa wahusika picha kimazingaombwe ni kitushi kinachomhusu Bi M, mkewe Ndi-, katika dondoo lifuatalo:

> Ghafla nilimwona Bi M akinyanyuka penye albamu nililokuwa nikilitazama. Na kawaida nilipotazama ukurasa huo, Bi M alianza tena kulirudia tendo lililokwishapita kwa miaka. Nadhani hata yeye lilimwathiri sana. Aaaa, nisiseme uwongo! Sikuwa na hakika kama picha ndiyo iliyoinuka au mwili, damu na mifupa (Mohamed, 2006:20).

Usawiri wa Bi M katika dondoo hili unakiuka misingi ya uhalisia. Bi M anaibuka ghafla kutoka kwenye albamu na kuwa kiumbe hai aliye na uwezo wa binadamu wa kawaida. Mipaka baina ya uhalisia na mazingaombwe inavunjwa na kukiukwa katika uumbaji wa mhusika huyu. Uhalisia na mazingaombwe yanasawiriwa kama matukio ya kawaida katika jamii na yasiyoweza kutenganishwa. Matukio haya

hutokea pamoja bila kutenganishwa. Hii ina maana kuwa usawiri wa wahusika unazingatia hali hizi mbili kwa pamoja.

Wahusika wengine ni wa kawaida japo wanasawiriwa kuwa na uwezo usiokuwa wa kawaida. Mfano mmojawapo ni ule wa mwanamke anayesubiri pamoja na Ndi- kwenye foleni kumwona daktari na kisha anajigeuza ghafla na kuwa hayawani, mwenye uso wa kiboko na manyoya ya mbuzi (uk. 86). Vilevile, Kilua, bintiye Ndi- ana uwezo wa kupenya akili na nafsi za wahusika wengine. Kilua anapokufa karibia mwisho wa hadithi baada ya kushambuliwa na nduguye Jitu, huo sio mwisho wa uhai wake Kilua. Kilua anazaliwa tena akiwa Bisudi, kitoto kilichopania kufumua jamii nzima kwa roho jagina ya kimapinduzi. Bisudi (Kilua aliyefufuliwa), akiwa na umri wa miezi mitatu tu anaweza kusema na kusoma kwa ufasaha bila kufundishwa kufanya hivyo.

## 5.0 Usimulizi

Mtindo wa kiusimulizi wa riwaya ya *Dunia Yao* unaonyesha ubunifu mkubwa wa mwandishi. Kwa mfano, kuna maingiliano baina ya sauti ya kisimulizi na mhusika, mvunjiko wa mkondo wa usimulizi na uchangamano wa kimuundo. Kuhusu mkakati wa usimulizi, kwenye riwaya hii mwandishi ametumia msimulizi wa nafsi ya kwanza na kuipa kazi yake mwonjo wa kitawasifu. Ndi-, ni msimulizi na wakati huohuo ni msimuliwa; kwa hivyo, yeye ni dira inayoelekeza mkondo wa hadithi hii japo kwa utata. Mwanzoni mwa usimulizi Ndi- anajieleza kwamba ndani yake mna watu wawili wanaowasiliana, “Ndi-mimi na -Ye ni yeye” (Shaib aliyekuwa zamani ndani ya nafsi yake Ndi-) na hivyo kuashiria uwili, uchangamano, utengano wa kiutu, na vilevile kuvunjika au kusambaratika kwa utambulisho, ambapo si dhahiri sana kubaini kama Ndi- anayeweza kuwa Ndimi tu au pia ni Ndiye. Yamkini utengano wa baadaye ndio unaochangia Ndi- na -Ye kubaki jina au majina yasiyokamilika yanayoishia au kuanzia kwa kistari na hivyo kutatiza badala ya kufafanua utambulisho kamili wa mhusika au wahusika.

Usimulizi wa *Dunia Yao* unaonyesha tabia ya kukwepa mtiririko wa moja kwa moja na sahili wenye kufuata mantiki. Ni usimulizi wenye kuoanisha sauti mbalimbali katika mkondo changamani usioshikana kabisa na mantiki ya wakati na pahala kama hadhira zetu zilivyozoea. Njia kuu ya usimulizi wa *Dunia Yao* kwa mfano, ni ile ya kuyamwaga na kufululiza matukio, mawazo, falsafa na siasa, visaasili, historia, dini na kuyaacha yashikamane na mtiririko wa hadithi bila ya kiungo bayana cha ploti kupitia visababisho na athari za visababisho katika mtiririko wa wakati na mahali. Matokeo ya mpiko huu wa mawazo ya falsafa, siasa na matukio ya hadithi yanayofululiza, ndiyo hatimaye yanakuwa kiini cha maudhui ya riwaya hii.

## 6.0 Dhana ya Wakati

Dhana ya wakati katika muktadha wa utandawazi imejadiliwa na Kezilahabi (2006) kwa kina. Mtaalamu huyu anabainisha dhana nne za wakati ambazo kwa

kiasi kikubwa zinaambatana na vyote vilivyomo ulimwenguni. Dhana hizi ni: Dhana ya mstari sambamba, dhana ya mviringo, dhana dhanaishi na dhana ya mabadiliko. Katika *Dunia Yao* mwandishi anaishughulikia dhana ya wakati kifalsafa. Kuhusu dhana ya wakati wa mstari sambamba, maneno kama 'maendeleo', 'kupiga hatua mbele' hutumika. Lakini maswali anayoyaibua mwandishi ni kuwa katika dunia ya utandawazi anayoisawiri tunapiga hatua mbele kwenda wapi? Kuna kasi, kasi isiyozuilika lakini tunakimbilia wapi? Mbele ni wapi? Je, saa kifaa kilichozoeleka cha kupima majira kinafaa kutumika tena wakati kimeelemewa na kasi ya mambo? Wakati unatusogeza wapi? Dhana ya wakati iko wapi? Akilini au kwenye uso wa saa na akrabu zake? Dondoo lifuatalo linaakisi taswira kamili ya hali hii:

> ... sijui lini lakini. Mwaka gani? Mwezi gani? Siku gani? Saa?...wakati hauwaziki tena. Mashiko hauna. Mantiki umeachana. Umepoteza maana! Saa inatikatika mezani. Inasonga mbele. Aaaa saa! Chombo tu na nambari zake. Ishara ya jinsi wakati unavyokupuka. Kasi, kasi...kasi isiyozuilika! Lakini mbele ndiyo wapi? Na nyuma ndiko kupi? Ninavyojua mimi, wakati una kiti chake kichwani. Si juu ya uso wa saa. Na siku hizi umefinywa mno...(Mohamed, 2006:1).

Wakati unaosawiriwa katika dondoo hili ni wakati wa kifalsafa. Hii ina maana kuwa haiyumkiniki wakati ulianza lini na utamalizika lini. Wakati huu hauwezi kuwekwa kwenye ncha mbili za mwanzo na mwisho wala kuwekewa vipimo vya saa, mwezi na mwaka. Isitoshe, wakati wa aina hii unaendelea kumsogeza mtu mbele japo haijulikani wapi anakokwenda au hadi lini. Mhusika Ndi anasafirishwa mbele na majira ya wakati bila hiari yake mwenyewe.

Mwandishi ameshughulikia dhana ya wakati wa mabadiliko katika muktadha wa utandawazi kwa kuonyesha mabadiliko katika jamii yaliyosababishwa na utandawazi. Jamii ya sasa inakabiliwa na mabadiliko yanayosababisha uchafuzi wa mazingira, kudorora kwa uchumi wa mataifa, mabadiliko ya siasa za ulimwengu na mabadiliko ya tabia yanayozua masuala ya kimaadili. Wazo kuu analolisisitiza mwandishi ni kuwa mabadiliko ni sehemu ya maisha; huwezi kumtenga binadamu na mabadiliko. Dhana ya wakati dhanaishi inaibuka wakati mwandishi anaposhugulikia hali ya binadamu kuwako katika dunia ya utandawazi. Mwandishi anasisitiza wazo kuwa tunauishi wakati lakini u kimya, unatuelekeza tusikokujua bila hiari yetu. Wakati unalinganishwa na gurudumu kwenye mwinamo mkali. Taswira hii inaakisiwa kwenye dondoo lifuatalo:

> Sina hakika ya mchana wala usiku. Wakati-mteremko wa gurudumu kubwa kwenye mwinamo mkali kuelekea gizani kunako giza ya kudumu...(uk. 28).

Dhana ya wakati unaosawiriwa katika dondoo hili ni ule usiorudi nyuma na unamwelekeza binadamu katika mauti kwa kasi ajabu. Wakati huu unasheheni ukimya na unamwelekeza binadamu katika maangamizi. Lengo la kutumia wakati

huu ni kuangaza taathira za kimaangamizi zinazonasibishwa na utandawazi. Binadamu anaelekezwa kwenye mauti yanayomsubiri na nguvu za utandawazi asizoweza kuzidhibiti.

Wakati mviringo umetumiwa na mwandishi kuonyesha kuporomoka kwa wakati. Wakati umevunjikavunjika; hakuna mwanzo wala mwisho. Kwenye riwaya wakati hauwezi kuwekwa kwenye ncha mbili za wakati. Wahusika wanaishi sasa, jana na kesho. Mwandishi anawatumia wahusika wanaosimulia matukio yaliyotendeka kitambo, matukio ya sasa na yale ya baadaye. Mwanzo wa riwaya hii hauhusiani na wakati na pahala maalum, lakini ni kituo cha nukta ya duara. Na hata mbele katika simulizi dhana ya wakati na mahali imeganda kabisa. Taswira hii inajitokeza kwenye dondoo lifuatalo:

> Sina hakika kama tunarejea nyuma au tunasonga mbele. Au pengine tunarejea nyuma huku tunaamini tunakwenda mbele... (Mohamed, 2006:177).

Wakati unaobainika katika dondoo hili ni wakati uliodumaa. Wakati umesimama na haijulikani iwapo kuna kurudi nyuma au kwenda mbele. Wakati huu unaweza kwenda upande wowote ule. Kwa mfano mhusika msimulizi anasimulia matukio yaliyotendeka kitambo, yale ya wakati wa kusimulia na hata yatakayotendeka baadaye. Uvunjwaji wa ncha mbili za wakati, yaani mwanzo na mwisho unalenga kuonyesha utata wa kuuhusisha utandawazi na kipindi maalum cha wakati.

## 7.0 Hali ya Ujirejelevu

Ujirejelevu ni dhana inayorejelea sifa ya kazi ya fasihi kuvuta makini kwenye hali yake ya kuwa kazi iliyotungwa au kubuniwa. Sifa hii ya ujirejelevu inaweza kuuweka mpaka au umbali kati ya msomaji na matukio yaliyoko kwa kumkumbusha msomaji kuwa anaopambana nao ni wahusika tu (Wamitila, 2003). Hali ya ujirejelevu hutawala katika uandishi unaotumia njia ya usasabaadaye kubuni kazi ya fasihi. Msimulizi katika kazi ya kibunilizipiku au metabunilizi husimulia kuhusu zoezi la uandishi au utunzi wa kazi za fasihi. Matumizi ya mbinu za kibunilizipiku hutokana na hitaji la jamii ya kisasa la kutaka kudadisi dhana ya uhalisia na kutathmini au kukadiria umuhimu wake katika dunia ya sasa iliyoathiriwa na utandawazi.

Waugh (2002) anaeleza kuwa istilahi metabunilizi au bunilizipiku inatumiwa kurejelea kazi za fasihi ambazo zinabainisha hali ya ujirejelevu. Waugh anaeleza kuwa kazi za aina hii huelekeza msisitizo kwenye hali yake ya kuwa kitu kilichobuniwa ili kudadisi uhusiano uliopo kati ya ubunifu na uhalisia. Licha ya haya, metabunilizi hutalii nadharia ya kutunga au kusanii bunilizi kupitia kwenye zoezi halisi la uandishi wa bunilizi. Hali hii inajitokeza kwenye riwaya ya *Dunia Yao*, mwandishi anasimulia kuhusu uandishi wa riwaya kwa misingi ya usasabaadaye unaohusu kuvunja kanuni za lugha, kujenga maana kwa njia ya kubomoa maana, kupoteza maana katika vivuli vya maana, kuunga vipande visivyoshikana katika masimulizi na kuyafanya maneno kuwa wahusika, picha,

watu, mashetani, wanyama au vivuli. Taswira hii inabainika wazi katika dondoo lifuatalo:

> Katika kubuni na kuumba-Bi Muse anapokujia na kukuchota kwa uzuri wake-kama koja la ajabu, unatunga sauti na sauti; ileile au tofauti, na kupata silabi. Silabi na silabi, unapata neno! Neno, maneno. Ibara na sentensi huzaa matini. Na vyote hivyo ni sehemu ya simulizi-maandishi...(Mohamed, 2006:9).

Kupitia kwa sauti ya mhusika msimulizi kwenye dondoo hili mwandishi anafichua kuhusu usimulizi wa riwaya ya *Dunia Yao*. Sifa hii inaipa riwaya hii sura ya ujirejelevu. Mwandishi anadokeza kuhusu muundo wa riwaya, usimulizi wake, madhumuni ya uandishi wake, matumizi yake ya lugha na hata usawiri wa wahusika waliotumiwa. Hali hii humsaidia msomaji kupata mwao kuhusu hali ya uchangamano wa riwaya.

Katika riwaya ya *Dunia Yao* mwandishi ametumia hali ya ujirejelevu kama mbinu ya kumtanabahisha msomaji kuhusu njia za utunzi wenyewe. Riwaya yenyewe inatoa maoni kuhusu usimulizi wake na njia za kubuni na kutunga riwaya. Kimsingi, *Dunia Yao* ni riwaya inayofichua mbinu zake za kiutunzi. Kwa mfano mazungumzo baina ya Ndi- na Ye-, yaani Shaib, kuhusu baadhi ya mbinu zenye mnasaba na usasabaadaye zinazotumiwa katika uandishi wa riwaya anayoiita *Dunia Yao*. Hali hii inajitokeza kwenye dondoo lifuatalo:

> ‘‘Unafikiri kitakusaidia katika riwaya yako ya *Dunia Yao*?’’
> ‘‘*Intertexuality...mchanganyondimi* unakusudia?’’ Nilicheka (Mohamed, 2006:68).

Dondoo hili linafichua kwamba mwandishi ametumia mwingilianomatini na mchanganyondimi katika usimulizi wake. Msomaji anaweza kubainisha haya kupitia kwa sauti mbalimbali zinazoshiriki katika usimulizi unaohusu matukio na visa vya kihistoria, kifalsafa, kisiasa na kidini.

## 8.0 Mwingilianomatini

Ndani ya riwaya ya *Dunia Yao* mna mwingiliano mwingi wa historia, kwa mfano, historia za waandishi na wahusika wao, historia ya dunia, historia ya ukandamizaji, historia ya ukombozi, historia za matini, na historia za tanzu za fasihi. Mwandishi anazingatia historia ya dunia kuanzia Vita vya Kwanza vya Dunia hadi sasa wakati ambapo kumekuwa na uvamizi wa magaidi wa kimataifa. Taswaira hii inabainika kwenye dondoo lifuatalo:

> Nilijikuta nachupia maiti waliolala kwenye midani ya mapambano ya Vita vya Kwanza vya Dunia. Na vilipokuja Vita vya Pili vya Dunia nikajiona...Tena vikanijia vipande vya mambo mfululizo. Nikavimeza. Vipande vya vita vya Ghuba vilinitibua roho. Vipande vya ‘sanctions’ kwa Iraki vilinikata maini...Kolombia. Peru. Meksiko. Yugoslavia. Bosnia...(Mohamed, 2006:45).

Katika dondoo hili mwandishi anazingatia siasa za ulimwengu kwa kurejelea matukio mawili yaliyoathiri historia ya dunia. Matukio hayo ni Vita Vikuu vya

Kwanza na vya Pili vya Dunia. Mchango wa Marekani katika vita hivyo na vita vya baadaye hususan vile vya Ghuba la Uajemi unasimuliwa. Lengo la mwandishi ni kuonyesha uwezo wa Marekani wa kivita unaowafanya kuvamia na kudhibiti mataifa mengine duniani.

## 9.0 Umbo la Riwaya

Umbo la riwaya mpya ya Kiswahili kwa kiasi fulani limegeuzwa makusudi. Mwandishi ametumia sanaahati inayodhihirika kwa njia zifuatazo: hati-mlalo, hati-kozefu, udogowesho, na ukuzaji wa herufi, lengo likiwa kusisitiza hali ya kukosa utambulisho na mporomoko wa kila kitu. Mifano ya matumizi ya sanaahati inabainika katika madondoo yafuatayo:

> Kompyuta **ha**kuwa mtatuzi kamili kwa hakika, kwani **a**lihitaji kulishwa (matumizi ya hati kozefu) (uk. 11)
>
> - Kufungua albamu...
> - Kufungua mziki.... (matumizi ya nukta) (uk. 11)
>
> **WeWe** ndani ya ***mimi***... (ukuzaji wa herufi na udogowesho) (uk. 22)
> **Cider** labda aina ya **nonentity** (matumizi ya udogowesho) (uk. 29)
> < *Unyamavu wa Yungi masikini*> (matumizi ya mabano yaliyopinda) (uk. 151).

Aidha, katika riwaya hii alama mpya za kauli zinasemwa moja kwa moja, kuna sura fupi mno kiasi cha aya tatu nne hivi, sura ndefu zenye kurasa 20 hivi au zaidi, mianzo kufungamana na mwisho katika mtindo wa ukamilishaji riwaya, mazungumzo yanayopangwa kwenye sura kama vile yanatokea kwenye tamthiliya, kukatwa maneno na uvunjaji wa kanuni za kisarufi.

## 10.0 Hitimisho

Makala hii imezungumzia taswira za utandawazi katika riwaya mpya ya Kiswahili hususani *Dunia Yao*. Masuala mbalimbali yameangaziwa na kuonesha namna yanavyoakisi utandawazi. Hii ni pamoja na dhamira, lugha, wahusika, wakati, hali ya ujirejelevu, mwingilianomatini na umbo la riwaya. Taswira za utandawazi wa riwaya ya *Dunia Yao* zimo katika usanii na maudhui yake. Kisanaa kuna mabadiliko mengi ya kushangaza na kutatiza. Baadhi ya mabadiliko hayo yanahusu muundo na vitomeo vyake vya fani na umbuji katika mbinu inayojaribu kuasi kwa makusudi uhalisia mkongwe. Mbinu ya uhalisiamazingaombwe inajitokeza katika kila kipengele cha riwaya hii mpya iwe usimulizi, uhusika, mwingiliano wa wahusika na hali za kisaikolojia ndani ya vichwa vyao. Isitoshe, kuna ndoto zinazoingiliana na ukweli wa mambo, matukio katika mshikamano wa uzoefu na ugeni wa mambo, mazingira na jinsi yanavyoshikana na matukio na kufungamana na wahusika kihistoria; umataifa, usayansi na mabaki ya uchawi, ushirikina na mazingaombwe. Hatimaye kuna mwingilianomatini na mchezo wa lugha unaofanya wakati mwingine hata kuingia katika uga wa kimetafizikia na

metabunilizi au bunilizipiku. Kwa hiyo, tunapoichanganua riwaya hii kuna haja ya kuiweka kwenye muktadha wa utandawazi ili kuielewa vizuri.

**Marejeleo**


Batibo, H. M. (2006). "Kiswahili na Lugha Nyingine za Afrika katika Ulimwengu wa Utandawazi," katika S. Sewangi na J. Madumulla (Wah.) *Makala ya Kongamano la Kimataifa la Jubilei ya TUKI – 2005: Kuadhimisha Miaka 75 ya Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (1930 – 2005).* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, kur. 96-104

Chachage, C. L. (2002). *Makuadi wa Soko Huria*. Dar-es-Salaam: Dar-es-Salaam University Press.

Gromov, M. D. (2004) "Post-modernistic Elements in Recent Kiswahili Novels," in *The Nairobi Journal of Literature*: The Journal of the Department of Literature, University of Nairobi, 2: 28-360.

Kezilahabi, E. (2006). "Utandawazi, Kiswahili na Dhana ya Wakati," katika S. Sewangi na J. Madumulla (Wah.) *Makala ya Kongamano la Kimataifa la Jubilei ya TUKI – 2005: Kuadhimisha Miaka 75 ya Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (1930 – 2005).* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. kur. 164-172.

_____(1990). *Nagona*. Dar-es-Salaam: Dar-es-Salaam University Press.

_____(1990). *Mzingile*. Dar-es-Salaam: Dar-es-Salaam University Press.

Khamis, S. A.M. (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta University Press.

_____(2004). "Utandawazi au Utandawizi: Jinsi Riwaya Mpya ya Kiswahili Inavyodai," katika *Jarida la Kiswahili* Juzuu 70. Dar es Salaam: TUKI, kur.47-66.

_____(2006). *Dunia Yao*. Nairobi: Oxford University Press.

_____(2008). ''Nadharia, Ubunifu, Uchambuzi na Taaluma ya Kiswahili,'' katika N. O. Ogechi na wenzie (Wah) *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*. Eldoret: Moi University Press. kur. 3-25.

Masele, B. (2006). "Kutandawaza Lugha Pendwa kwa Kutunduwaza Lugha Fakiri," katika S. Sewangi na J. Madumulla (Wah.) *Makala ya Kongamano la Kimataifa la Jubilei ya TUKI – 2005: Kuadhimisha Miaka 75 ya Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (1930 – 2005).* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. kur. 156-163.

Mkangi, K. (1995). *Walenisi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mkufya, W. E. (1999). *Ziraili na Zirani*. Dar-es-Salaam: Hekima Publishers.

Mulokozi, M. (2006). "Fasihi ya Kiswahili na Utandawazi" katika S. Sewangi na J. Madumulla (Wah.) *Makala ya Kongamano la Kimataifa la Jubilei ya TUKI – 2005: Kuadhimisha Miaka 75 ya Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (1930 – 2005).* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Ruigrok, W and R Van Tulder. (1995). *The Logic of International Restructuring*. New York: Routledge.

Simala, I. (2006). "Fasihi Simulizi katika Enzi ya Utandawazi," katika Njogu, K. na wenzie (wah.) *Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Nairobi: Twaweza Communications.
kur. 11-18.

Wafula, R. na Njogu, K. (2007). *Nadharia na Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers.

_____(2002). *Bina-Adamu!* Nairobi: Phoenix Publishers.

_____(2004). *Musaleo!* Nairobi: Vide~Muwa Publishers.

_____(2007). *Dharau ya Ini*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers.

_____(2008). *Unaitwa Nani*? Nairobi: Vide~Muwa Publishers.

Waugh, P. (2002). *Metafiction: Theory and Practice of Self Conscious Fiction*. London: Routledge.